

# MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA MJINI MOSHI



## UVUJAJI WA MAJI

Uvujaji wa Maji Safi hutokea mara nyingi kwenye maeneo na sehemu nyingi katika Bomba za Wateja wa Huduma ya Maji Safi na kusababisha:

- Upotevu na hasara kubwa kwa rasilimali ya maji nchini mwetu na duniani kote,
- Uharibifu mkubwa wa mazingira na hatimaye kuchangia kwa kiasi kikubwa katika milipuko ya magonjwa ya kuambukiza,
- Ongezeko la deni katika ankara ya Mteja ya kila mwezi na kulazimika kulilipa ili kuendelea kupata Huduma ya Maji Safi na Salama.

Uchakavu wa Bomba za Maji Safi na Salama ndio Chanzo kikuu cha Uvujaji wa Maji katika Manispaa ya Moshi, Mji wetu wa Mlima Kilimanjaro!

Ni jukumu la Wateja wa Huduma ya Maji Safi, Wakazi wa Mji wa Moshi na Mamlaka kuhakikisha kuwa uvujaji hautokei na kuachwa kuendelea ili kulinda Afya zetu, Mazingira yetu na Kuhifadhi kiasi cha maji ambacho kihistoria hupungua kila siku.



Ni Jukumu la Mteja wa Huduma ya Maji Safi kuhakikisha kuwa:-

1. anagundua Uvujaji wowote wa Maji katika Bomba zake, Kabla na Baada ya Dira ya Maji ama Ndani ya Nyumba yake kwa kushuhudia kirahisi mzunguko wa Dira ya Maji hata kama maji hayatumiki kwa wakati huo,
2. anatoa Taarifa ya Uvujaji wa Maji kwa Mamlaka ili kupata ushauri wa jinsi ya kudhibiti Uvujaji katika Eneo ama Nyumba yake,
3. anadhibiti Uvujaji katika Bomba lake kwa kufanya Matengenezo yote yanayostahili.

#### **TAHADHARI:**

---

- Iwapo Mteja hatadhibiti Uvujaji wa Maji katika Bomba zake, Mamlaka italazimika kusitisha (kukata) Huduma ya Maji katika Eneo ama Nyumba husika hadi Uvujaji utakapodhibitiwa.
  - Mteja atalazimika Kulipia Ankara ya Maji ambayo itatokana na uzembe wake wa kutodhibiti Uvujaji wa Maji katika Bomba lake.
- 

Kwa Upande wake, Mamlaka inahakikisha kuwa inadhibiti Uvujaji wa maji utakaojitokeza wakati wowote katika Bomba Kuu za kusambazia maji ili kuepuka madhara yatokanayo.

Kwa Maelezo zaidi, Kutoa Taarifa ama Kuomba Ushauri Mteja atapaswa kuwasiliana na Kitengo cha Mahusiano na Wateja (Huduma kwa Wateja).

**Sote Tuitunze Rasilimali ya Maji kwa Uhai wetu!**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA  
MJINI MOSHI**

**S.L.P 324, MOSHI Simu: 2751164  
Barua Pepe: muwasa@kilionline.com**